

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **WITO KWA UMMA KUTOA MAONI JUU YA MAPENDEKEZO YA KANUNI NA MWONGOZO KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI MIDOGO MIDOGO YA KUZALISHA UMEME KATIKA TANZANIA**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) iko katika mchakato wa kuandaa mfumo wa udhibiti utakaosaidia katika uanzishaji wa miradi midogo midogo ya umeme (Small Power Projects – “SPP”) sambamba na sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2003 katika kuhamasisha wawekezaji binafsi kuwekeza katika miradi midogo midogo ya umeme hapa Nchini. Kama hatua ya kwanza, EWURA iliridhia mkataba maalumu wa kuuziana umeme usiozidi Megawatt 10 (Standard Small Power Purchase Agreement – “SPPA”) na mfumo wa kukokotoa bei ya umeme huo (Standardised Tariff Methodology) kwa aina hiyo ya miradi itakayotumia nishati jadidifu pamoja na umeme wa mabaki ya mimea au mazao viwandani yaani “cogeneration”. EWURA iko katika hatua za mwisho za kutengeneza kanuni (rules) na mwongozo (guidelines) ili kukamilisha utaratibu utakaofuatwa katika mfumo huo. Malengo ya mfumo huo ni kurahisisha uwekezaji katika miradi hiyo midogo midogo. Mfumo huo utakapoanza kutumika utaleta faida nyingi zikiwemo kupata vibali mbali mbali kwa haraka kutoka katika mamlaka husika, kupunguza kwa kiasi kikubwa majadiliano na mnunuzi wa umeme, kupunguza mahitaji yanayofanana kutoka mamlaka mbali mbali, kuondoa urasimu na kuwezesha maamuzi ya haraka kutoka kwa utumishi wa Umma. Aidha, mfumo huu unategemewa kuweka chachu, sio tu katika kuhamasisha ushiriki wa wawekezaji binafsi katika sekta ya nishati, bali pia katika uendelezaji wa vyanzo vya nishati jadidifu (renewable energy) na kuharakisha nishati ya umeme kuwafikia wananchi walio wengi huko vijijini.

Mfumo huu utaweka msingi wa kisheria wa kuwawezesha wajasiliamali kuwekeza katika miradi midogo midogo ya kuzalisha umeme utokanao na nishati jadidifu na kuuza umeme huo kwenye gridi ya taifa au gridi ndogo kiasi kisichozidi Megawatt 10. Mahali pengine, miradi hiyo itaondoa mahitaji ya mafuta ya dizeli kuzalishia umeme.

Hivyo, kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(b) cha sheria namba 414, EWURA sasa inawatangazia wadau wote wa umeme na wananchi kwa ujumla kusoma na kutafakari rasimu ya kanuni na mwongozo zilizotajwa hapa chini, na kisha kutoa maoni yao kwa maandishi ili kuboresha mfumo unaopendekezwa. Maoni ya maandishi yawasilishwe kwa Mkurugenzi Mkuu kupitia anwani iliyooneshwa hapo juu wakati wa saa za kazi (saa 2.00 asubuhi hadi 11.00 jioni) au kupitia Barua Pepe: [electricity@ewura.go.tz](mailto:electricity@ewura.go.tz). Mwisho wa kupokea maoni hayo ni tarehe 6/9/2010.

- (1) *The Electricity (Development of Small Power Project) Rules, 2010,*
- (2) *The Small Power Project development guidelines comprising of*
  - i. *Procedural Requirements for various consents, and*
  - ii. *Technical and Safety Requirements for interconnection.*

Makabrasha yenye kanuni na mwongozo kama yalivyotajwa hapo juu yanapatikana bure kwenye tovuti ya EWURA ([www.ewura.go.tz](http://www.ewura.go.tz)), au kutoka ofisi za EWURA kwa gharama ndogo ya Sh. 25,000 ili kufidia gharama za kudurufu makaburasha hayo, baada ya kuleta maombi kwa maandishi.

Kwa ufafanuzi zaidi mwandikie Mkurugenzi Mkuu, EWURA kupitia anwani iliyoneshwa hapo juu, na Aione:

**Eng. Anastas P. Mbawala; Barua Pepe: ([mbawala@ewura.go.tz](mailto:mbawala@ewura.go.tz))**

**Imetolewa na:  
Mkurugenzi Mkuu,  
EWURA**